# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**HOTUBA YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, BAADA YA UKAGUZI WA MIRADI YA UJENZI WA KIWANJA CHA NDEGE CHA KIMATAIFA CHA MSALATO, NA BARABARA YA MZUNGUKO YA NJE YA JIJI LA DODOMA (km 112.3), ENEO LA NALA, DODOMA TAREHE 14 JUNI, 2025**

**(CORRECTED)**

- *Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete;*
- *Mheshimiwa Dkt. Akinwumi Ayodeji Adesina, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika;*
- *Mheshimiwa Abdallah Ulega, Waziri wa Ujenzi;*
- *Waheshimiwa Mawaziri mliopo;*
- *Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi;*
- *Dkt. Patricia N. Laverley, Meneja Mkazi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika;*
- *Mheshimiwa, Rosemary Sitaki Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;*
- *Ndugu Adam Kimbisa, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma;*
- *Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu;*
- *Waheshimiwa Wabunge Mliopo;*

- ***Balozi. Mhe. Aisha S. Amour Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi;***
- ***Makatibu Wakuu wengine mliopo;***
- ***Katibu Tawala wa Mkoa Dodoma;***
- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;***
- ***Wenyeviti wa Bodi za Taasisi za Wizara ya Ujenzi;***
- ***Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Madiwani;***
- ***Viongozi wa Serikali;***
- ***Viongozi wa Dini;***
- ***Viongozi wa Vyama vya Siasa;***
- ***Ndugu Wanahabari;***
- ***Wageni Waalikwa;***
- ***Mabibi na Mabwana;***

*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*!

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kujumuika mahali hapa.

Kukusanyika kwetu leo hapa ni kwa madhumuni ya kutoa shukrani na kumuaga Ndugu na Rafiki yetu Dkt, Akinumwi Adesina, Rais wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) anaemaliza muda wake wa utumishi katika benki hio. Mniruhusu nimshukuru kwa kuitikia mwaliko wetu na kuja kufanya ziara nchini wakati huu. Nimefurahi pia kumuona Meneja Mkazi wa AfDB hapa nchini, Dkt. Patricia Laverley ambaye amekuwa akishirikiana na Serikali kwa karibu sana. ***Karibu sana!***

***Ndugu zangu,***

Muda mfupi uliopita, tulifanya ziara ya kutembelea Barabara ya mzunguko inayojengwa ndani ya Mji wetu wa

Dodoma, na vile vile, tulikwenda kuona maendeleo ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, na Wizara yako kwa ujumla kwa kazi mnayoifanya ya kufuatilia utekelezaji wa miradi hii ambayo imefikia hatua nzuri ya utekelezaji.

Aidha, nakushukuruni wakazi wa Nala na Dodoma kwa ujumla kwa kujitokeza kwa wingi katika tukio hili. **Dodoma Oyee...!**

***Mihanyeni? (- Misaa);***

***Milimoni? (- Miswanu);***

***Chikulumba! (asante).***

***Asanteni sana.***

***Ndugu Wananchi,***

Benki ya Maendeleo ya Afrika imekuwa mbia mkubwa wa kutegemewa katika safari yetu ya maendeleo. Kipekee, katika kipindi cha uongozi wa ndugu yetu Dkt. Adesina, tumeshuhudia miradi mingi ya maendeleo ikitekelezwa kwa

fedha kutoka AfDB. Miradi hii imesaidia sana katika kuifungua na kuiunganisha Tanzania kwa njia za barabara, anga na reli. Halikadhalika, iko miradi mingine mingi katika sekta mbalimbali, ikiwemo kilimo na nishati; kote huko AfDB wametuunga mkono kikamilifu. Ndiyo maana leo nilimwomba Mheshimiwa Adesina atembelee baadhi ya miradi ili ajionee matunda ya kazi yake nzuri.

Uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Adesina umeleta manufaa na kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii, siyo tu hapa nchini, bali pia ndani ya Afrika kwa ujumla. Kwa kutambua mchango wake huu mkubwa, jana Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilimtunuku Shahada ya Udaktari wa Heshima katika taaluma za Sayansi. Nitumie fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Dkt. Adesina kwa Heshima hiyo ambayo kwa kweli anaistahili. Kwa unyenyekevu kabisa, niushukuru uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chini ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, kwa

kutambua na kuthamini mchango wa Mheshimiwa Adesina katika maendeleo ya Taifa letu na Bara letu. **Ahsanteni sana.**

***Ndugu Wananchi,***

Takriban miaka 8 iliyopita, Serikali ilifanya maamuzi ya kutekeleza azma yake ya muda mrefu ya kuhamia rasmi Dodoma. Utekelezaji wa maamuzi hayo umekuwa na manufaa makubwa, umefungua fursa nyingi kwa wakazi wa Dodoma na mikoa jirani, na umechangia kupandisha hadhi Mkoa wetu wa Dodoma. Hata hivyo, jambo jema hili, limeibua haja ya kuliendeleza zaidi Jiji la Dodoma kuendana na hadhi yake kama Mji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na vile vile, kuondosha msongamano wa magari uliopo kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wakazi pamoja na shughuli za kiuchumi na kijamii, na hasa kwa kuwa Dodoma ni kiungo cha barabara kuu mbili. Moja ni barabara ya ushoroba wa kati kutokea Dar es Salama kupitia Dodoma kwenda Kanda ya Ziwa hadi nchi jirani za

Burundi, Rwanda, Uganda na DRKongo. Nyingine ni barabara kuu ya ukanda wa kaskani yaani "*the Great North Road*" inayounganisha mikoa ya nyanda za juu kusini na kaskazini kupitia Arusha, na vilevile ndio barabara inayounganisha Kenya na majirani zetu wa kusini Zambia na Malawi. Hivyo, ni rahisi kuona kuwa msongamano katika Jiji la Dodoma unavyoweza kuathiri biashara ndani ya nchi na ukanda mzima.

Ili kuondosha kadhia hiyo, tunahitaji kuwa na barabara ambayo itayawezesha magari makubwa na madogo yasiyokuwa na ulazima wa kuingia katikati ya Jiji la Dodoma kuweza kuendelea na safari, hivyo kupunguza muda na gharama za safari. Vilevile, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kiutawala, wakazi wa Jiji la Dodoma wanahitaji urahisi wa kutoka eneo moja hadi eneo jingine, ili kurahisisha shughuli zao.

Katika kukabiliana na changamoto hizo mbili, Serikali ilikuja na mradi huu wa Barabara ya Mzunguko wa Nje wa Jiji la Dodoma yenye urefu wa kilomita 112.3, ambayo leo, tumepata fursa ya kuona maendeleo ya ujenzi wa Barabara hii ambayo ni muhimu sana kwa Jiji na Mkoa wa Dodoma, na nchi yetu kwa ujumla.

***Ndugu Wananchi,***

Kwa kuwa Dodoma ndio Makao Makuu ya Nchi yetu, inatulazimu kuufungua Mkoa wa Dodoma kwa njia tofauti zote, zikiwemo reli na anga. Kwa usafiri wa anga, mahitaji yameongezeka sana, na yanatarajiwa kuendelea kuongezeka zaidi, jinsi shughuli za kiuchumi zinavyoongezeka. Pamoja na kwamba tulifanya maboresho madogo ya uwanja wa ndege wa Dodoma ili kuuongezea uwezo, ikiwemo kuuwezesha kufanya kazi masaa 24. Hata hivyo, kama mnavyofahamu, Uwanja wa Ndege wa Dodoma ni mdogo na upo katikati ya Jiji, hali inayosababisha kutoweza

kufanyiwa upanuzi ili kuongeza uwezo wa uwanja kupokea ndege kubwa zaidi. Ili kuongeza ufanisi wa huduma za usafiri wa anga, ni dhahiri kuwa kama Makao Makuu ya nchi kuna haja kubwa ya kuwa na Uwanja wa ndege wa Kimataifa.

Hivyo, nimefurahi kuona kuwa mradi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato unaendelea vizuri. Uwanja huu umejengwa kwenye eneo lenye ukubwa wa kutosha hali iliyotuwezesha kuweka miundombinu yote inayohitajika kukidhi mahitaji ya sasa na miaka mingi ya mbele. Kiwanja hiki kitaimarisha mtandao wa usafiri wa anga wa ndani na nje ya nchi, ikiwemo kukuza utalii.

Barabara hii ya mzunguko wa nje wa Jiji la Dodoma imenufaika kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka AfDB, jumla ya Shilingi bilioni 489.982, ambayo ni asilimia 85 ya gharama yote ya mradi. Serikali kwa upande wetu

tukichangia asilimia 15, ya gharama hizo. Ujenzi wa uwanja wa ndege umenufaika kwa mkopo wa Dola za Marekani milioni 272 kutoka AfDB, huku Serikali ikitoa Dola za Marekani milioni 58. Tunaishukuru sana AfDB, na nimefurahi kuwa leo Rais wa Benki yupo nasi kujionea kazi inayofanyika, na namna ambavyo kazi hii inakwenda kuimarisha uchumi wa nchi na kustawisha maisha ya watu. ***Tuwapigie makofi mengi sana wabia wetu!***

***Ndugu Wananchi,***

Napenda sasa kutumia fursa hii kuwapongeza Wakandarasi, Wahandisi Washauri, *TANROADS* pamoja na Wizara ya Ujenzi kwa kujitoa kwao kutekeleza na kusimamia miradi hii kikamilifu.

Nawashukuru wananchi na wakazi wa maeneo inayopita na kujengwa miradi hii kwa uvumilivu wao katika kipindi chote cha ujenzi, pamoja na ushirikiano wao katika

kufanikisha utekelezaji wa miradi hii. Bila shaka, kukamilika kwa ujenzi wa Barabara ya Mzunguko ya Dodoma na Uwanja wa Ndege wa Mslato ni kwa maslahi ya kila mmoja wetu kwani utarahisisha usafiri na usafirishaji wa mazao ya chakula na biashara, pembejeo na bidhaa nyingine mnazozalisha.

Kama alivyosema Waziri wa Ujenzi, kukamilika kwa Barabara hii kutaongeza fursa na kutarahisisha biashara mbalimbali katika Mkoa wa Dodoma na Mikoa jirani na kufanya Wananchi wake waweze kujiletea maendeleo. Mradi huu pia utachangia kuifanya Tanzania kuendelea kuwa kitovu cha biashara katika Kanda ya Afrika Mashariki. Hivyo basi, nawasihi wananchi mnaoishi kwenye maeneo haya, muweze kuzitumia fursa za kuwepo miradi hii muweze kuongeza uzalishaji na kipato chenu.

*Ndugu Wananchi,*

Kwa niaba ya Wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa dhati kabisa tutoe shikrani zetu kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kueendelea kuwa mdau mkubwa katika utekelezaji wa miradi ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege hapa nchini. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na:-

i) Barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu (km 260.6) ujenzi unaendelea na upo kwenye hatua za mwisho za utekelezaji;

ii) Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya II (km 20.3) ambapo ujenzi umekamilika;

iii) Barabara ya Mnivata – Newala – Masasi (km 160), ujenzi unaendelea;

iv) Barabara ya Namtumbo – Tunduru (km 193) ambapo ujenzi umekamilika;

v) Barabara ya Dodoma – Iringa (km 260) ambapo ujenzi umekamilika;

vi) Barabara ya Dodoma – Babati (km 188.15) ambapo ujenzi umekamilika;

vii) Barabara ya Sakina – Tengeru (km 14.1) pamoja na Barabara ya Mchepuo wa Arusha (km 42.4) ambapo ujenzi umekamilika;

viii) Barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) ambapo ujenzi umekamilika;

ix) Barabara ya Tunduru – Nakapanya – Mangaka – Mtamba Swala (km 202.5) ambapo ujenzi umekamilika; na

x) Barabara ya Tabora – Koga – Mpanda (km 342.9) ambapo ujenzi umekamilika.

Katika hatua nyengine, Benki ya *AfDB* ilitusaidia kuongeza upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wetu kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania.

***Benki ya AfDB Oyee..! Adesina Oyee..!***

Pamoja na kujionea utekelezaji wa miradi hii miwili ya barabara na uwanja wa ndege, leo Dkt. Adesina na ujumbe wake, alisafiri kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma kwa kutumia reli yetu ya *SGR*, na alijionea huduma zinazotolewa kwenye reli hiyo. Mradi wa *SGR* nao ni sehemu ya miradi inayoenda kuifungua Dodoma, na Tanzania kwa ujumla. Safari za abiria zilizoanza mwezi Agosti mwaka jana zimepunguza muda wa kusafiri kutoka takriban saa nane mpaka tisa kwa barabara, hadi wastani wa saa tatu. Aidha, tayari kumekuwa na majaribio ya kusafirisha mizigo, na muda wowote safari hizo zitaanza rasmi. Nafarijika kuwa Dkt. Adesina na ujumbe wake wameziona huduma za reli hii; kwani licha ya kuwa mradi huu tuliuanza sisi wenyewe

na kazi kubwa imefanyika na inaendelea kufanyika, mwaka juzi *AfDB* nayo imetuunga mkono kwenye vipande viwili vya mradi huu vinavyoenda kuunganisha reli hii na nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Ni kutokana na yote haya, nilitangulia kwa kusema kuwa *AfDB* imekuwa mbia wa kweli na mdau muhimu katika maendeleo ya miundombinu nchini Tanzania. Kwa niaba ya Watanzania, napenda kuishukuru tena *AfDB* kwa ushirikiano huu mkubwa katika kuendeleza miundombinu na kuchochea maendeleo zaidi hapa nchini. **Asanteni sana.**

Vilevile, sina budi kuwatambua na kuwashukuru pia, wale wote walioshiriki katika hatua za awali za mradi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato na tunaoendelea kushirikiana nao katika miradi mingine, hususan Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika (BADEA), Mfuko wa Maendeleo wa Kimataifa wa Shirika la Nchi Zinazozalisha

Mafuta Duniani (OFID) pamoja na mkandarasi *Arab Consulting Engineers* (ACE) kutoka Misri.

***Ndugu wananchi,***

Ninapoelekea kuhitimisha, nizitake Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi kuhakikisha kazi za Ujenzi na Ukarabati wa miundombinu ya Barabara, Reli na Viwanja vya Ndege inatekelezwa kwa viwango vilivyokusudiwa kimkataba. Vilevile, muwasimamie kwa karibu wakandarasi wote ili Barabara ya Mzunguko wa Nje ikamilike Mwezi Agosti mwaka huu 2025 na Uwanja wa Ndege wa Msalato mwezi Novemba, 2025 kama ilivyopangwa.

Kwa ndugu zangu wa Dodoma, mbali na kwamba barabara hii itakuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo, nawashauri kuandaa na kutekeleza mipango na mikakati ya kuipamba kwa mashamba ya kilimo cha kisasa, hususan kwa mazao ya alizeti na zabibu.

Kama nilivyosema, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafiri hugharimu fedha nyingi, hivyo ni muhimu sote tuitunze ili idumu kwa muda mrefu. Ulinzi wa mali za Taifa ni wetu sote, hivyo kila mwananchi awe mlinzi kwa mwenziwe. Misemo yetu ya busara inatuambia "**Kitunze Kidumu" au Kipendeze.**

***Ndugu Wananchi,***

Kama nivyotangulia kusema, katika ziara yangu hii, mmeona nipo na Dkt. Akinwumi Adesina, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), ambayo chini ya uongozi wake imetusaidia sana katika miradi mingi ya maendeleo. Dkt. Adesina anamaliza muda wake, kama Rais wa Benki ya *AfDB*, hivyo, napenda niongeze shukrani zangu za dhati kwa juhudi zake za kuisaidia Tanzania. Katika kumuwekea kumbukumbu, na kwa kutambua mchango wake na Benki ya Maendeleo ya Afrika katika kuimarisha sekta ya Usafiri na usafishaji Tanzania, nimeridhia pendekezo la Waziri wa

Ujenzi la kuwa Barabara hii iitwe jina lake**.** Hivyo, nami nawasilisha ombi hili kwenu na naomba mnikubalie, ili nitangaze rasmi kuwa Barabara hii ya Mzunguko wa Nje wa Jiji la Dodoma itaitwa **Barabara ya Dkt. Akinwumi Adesina**.

***Ndugu Wananchi,***

Mwisho kabisa, niseme kwamba Tanzania imeweza kuvutia mitaji kutoka kwa wabia muhimu kama *AfDB* kutokana na kuwepo kwa Utulivu na Amani, Sera nzuri za kiuchumi, usimamizi thabiti wa miradi mbalimbali ya maendeleo, na kujituma kwa Watanzania wenyewe kujenga nchi yao. Kwa pamoja, ***tumeendelea kuonyesha Afrika na dunia kwamba Tanzania imedhamiria kujenga taifa lenye uchumi shindani na kustawisha hali za maisha za Wananchi***. Hivyo, niithibitishie Benki ya Maendeleo ya Afrika, kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kuwa mshirika wa karibu na *AfDB* hata siku za usoni kufikia

malengo ya bara letu ya kujenga Afrika tunayoitaka, na kuleta maendeleo zaidi kwa watu wetu.

Baada ya kusema hayo, ninawashukuru sana kwa kunikisiliza.

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania..!***